# حَقِيْقَةُ يَوْمِ الْقُدْسِ

# UKWELI WA SIKU YA QUDSI

## NI IPI SIKU YA QUDSI?

Mashia kila inapfika Ijumaa ya mwisho ya mwezi wa Ramadhani, hutoka barabarani na kufanya maandamano kwa madai kwamba hiyo ni siku ya kuwatetea ndugu zetu Wapelestina na kutaka kuikomboa Yerusalem na Masjidul Aqsa.

Lakini uhalisia ni kinyume na madai yao, kwa sababu ukisoma ndani ya vitabu vyao vya kutegemewa utapata kwamba wao hawaitakidi kwamba msikiti huo uliopo Palestina ndio Masjidul Aqsa, bali Masjidul Aqsa iko mbinguni!

## JE NI KWELI MASHIA WANAWAPENDA NDUGU ZAO WAPELESTINA?

Madai haya si kweli, kwanza wangempenda Khalifa wa pili wa Waislamu Omar Ibnul Khataab -Allaah amridhie- ambaye alisimama madhubuti kuunusuru msikiti huo ambao leo Wapelestina wanautetea, mpaka Mayahudi wakajisalimisha kwake na kumkabidhi funguo zake?! Badala yake wanaona: **"Inafaa kusherehekea siku aliyouwawa Omar na kumzingatia mtu aliyemuuwa Omar ni shujaa…"[1].**

Na vipi watawanusuru watu wa Ghaza na hali ya kuwa si Mashia wenzao? Na miongoni mwa Itikadi za Shia ni kwamba Sunni kwao si Muislamu.

Hizi ni baadhi ya kauli za Maulamaa wao:

- **"Ni halali kumwaga damu ya Sunni…".** [Wasaailu Sshia] (Jz. 18, Uk. 463).
- **"Ni halali kuchukua mali ya Sunni popote utakapoikuta…"[2].**
- **"Sunni ni najisi tena ni kiumbe wa shari kuliko Yahudi na Naswara…"[3].**
- **Haifai Shia kuosha wala kumswalia maiti ya mtu asiyewakubali Maimamu 12…, na ikiwa hakuna budi basi atafanya kwa Taqiyya, atamuosha bila nguo na wakati wa kumswalia atamlaani wala hatomuombea dua (ya kheri)"[4].**

---

[1]- Kitabu: [Aqdu Ddurari fii baqri batni Umar] (Uk. 120). Cha Yasin As Swawwaaf.
[2]- Kitabu: [Wasaailu Sshia] (Jz. 6, Uk. 340). Cha Hurru al 'Aamiliy.
[3]- Kitabu: [Al Anwaaru Nnu'maaniyyah] (Jz. 5, Uk. 247-248). Cha Ni'matullaah Al Jazaairiy.
[4]- Kitabu: [Al Muqni'a] (Uk. 85). Cha al Mufid.

## JE MASJIDUL AQSA YA MASHIA IKO WAPI?

Imepokewa kwamba kijana mmoja alimuuliza Abu Abdillaah (As saadiq) kuhusiana na misikiti mitakatifu, akasema: **"Al Masjid al Haraam (Makka), msikiti wa Mtume -Swala na Salamu zimshukie- (Madina)".** Nikamuuliza: Je, msikiti wa Aqsa? Akajibu: **"Huo uko mbinguni, alipelekwa Mtume alaihis salaam katika usiku wa Israa".** Nikasema: Lakini watu wanasema msikiti huo ni Baytil Maqdis (Palestina), akajibu: **"Msikiti uliopo mji wa Kufa ni bora kuliko huo (Baytil maqdis)"**[5]. Angalia ndugu msomaji, Mashia wanaufadhilisha msikiti uliopo mji wa Kufa huko Iraq kuliko Al Masjid al Aqsa uliopo Palestina, bali wamepotosha mpaka maana ya hadithi inayojuzisha kufungia safari ya ibada Kwenda (Al masjidul Haram 'Makka', Al masjidu Nnabawi 'Madina', na Al masjidul Aqsa 'Palestina'), amesema sheikh wao As Saduq: **"Msifunge safari ya kiibada isipokuwa kwenda kwenye misikiti mitatu: Al masjidul Haraam, Msikiti wa Mtume -Swala na Salamu zimshukie- na Msikiti wa Kufa"**[6]**.** Zinduka ewe ndugu Muislamu…

Bali msikiti huo wa Kufa unauzidi mpaka msikiti wa Makka na Madina Amesema sheikh wao mkubwa Al-Kulayn: **"Swala moja katika msikiti wa Al-Kufa ni sawa na swala Elfu moja katika misikiti mingine usiokuwa huo"**[7]**.**

Kadhaalika Abbas al Qummi amesema: **"Lakini lenye kudhihiri katika hadithi nyingi ni kwamba makusudio ya Al masjidul Aqsa, ni Al baytul Ma'mour iliyopo katika mbingu ya nne, na huo ndio msikiti wa mbali (Masjidul Aqsa)"**[8]**.**

## Kutukuza kwao maeneo ambayo si matakatifu:

Imepokewa kutoka kwa Abu Abdillaah amesema: **"Ukitaka kwenda Hija halafu ikawa ni uzito kwako, basi fanya ziara kwenye kaburi la Hussein, (alaihis salaam), kwa sababu ukizuru kaburi la Hussein utaandikiwa malipo sawa na Hija, na ukitaka kufanya Umra kisha ukashindwa, basi fanya ziara kwenye kaburi la Hussein (alaihis salaam), utaandikiwa kwa ziara hiyo malipo ya Umra".** [Wasaailu Sshia] (Jz. 10, Uk. 332).

**Abu Halima Arafat**

**25/Ramadhani/1445H – 5/4/2024M.**

---

[5]- Kitabu: [Bihaaru al Anwaar] (Jz. 18, Uk. 385) cha Al Majlis.
[6]- Kitabu: [Al Khiswaal] (Jz. 1, Uk. 149).
[7]- Kitabu: [Mustadrak al Wasaail] (Jz. 3, Uk. 304).
[8]- Kitabu: [Muntahaa al Aamal] (Uk. 70) cha Abbas Al Qummi.